BENKI KUU YA TANZANIA



# TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia........1

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa........3

- 2.1 Uchumi wa Ndani........3
- 2.2 Mfumuko wa Ndai........3
- 2.3 Sera ya Fedha........5
- 2.4 Viwango vya Fedha........7
- 2.5 Masoko ya Fedha ........8
- 2.6 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali........9
- 2.7 Mwenendo wa Deni la Taifa ........9
- 2.8 Mwenendo wa Sekta ya Nje........11

3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar........14

- 3.1 Mfumuko wa Bei........14
- 3.1 Mfumuko wa Bei........13
- 3.2 Bajeti ya Serikali........14
- 3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje........15

Viambatisho........30

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliendelea kuimarika katika kipindi cha mwaka 2025, ukihimili misukosuko iliyotokana na hali ya kutotabirika kwa sera za kibiashara, kuongezeka kwa ushuru na mivutano ya kisiasa (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b). Kuimarika kwa uchumi wa dunia kuliyochagizwa na majadiliano ya kiabiashara baina ya nchi zenye ushawishi mkubwa wa kiuchumi, kuongezeka kwa matumizi binafsi, uwekezaji katika sekta zinazotumia teknolojia, masharti nafuu ya huduma za kifedha, pamoja na sera saidizi za uchumi jumla katika nchi zilizoendelea.

Kutokana na kasi ya ukuaji uchumi iliyoonekana mwishoni mwa mwaka 2025, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika taarifa yake ya Januari 2026 kuhusu mwelekeo wa uchumi wa dunia (World Economic Outlook Update) ilirekebisha maoteo ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 hadi asilimia 3.3, ikipanda kutoka makadirio ya asilimia 3.2 ya taarifa ya Oktoba 2025. Marekebisho haya ni madogo, lakini ya maana kwa matarajio ya muda mfupi. Hata hivyo, uchumi wa dunia umeendelea kukumbwa na vihatarishi vinavyoashiria uwezekano wa kushuka kwa ukuaji kutokana na kuongezeka kwa mivutano ya kibiashara, nakisi ya bajeti na madeni, pamoja na mivutano ya siasa za kimataifa[1].

[1] Taarifa ya IMF kuhusu Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia, Januari 2026

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya kutokuwa na uhakika wa sera za dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya kutokuwa na uhakika wa biashara duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Bei za bidhaa katika soko la dunia zilikua na mwelekeo mchanganyiko kwa mwezi Desemba 2025. Bei ya mafuta ghafi ilishuka, hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 61 kwa pipa, hali iliyochangiwa na ongezeko la ugavi sambamba na kupungua kwa mahitaji, hususan kutoka China na India. Bei ya dhahabu iliendelea kuongezeka na kufikia dola za Marekani 4,309 kwa wakia mwezi Desemba 2025, kutokana na kuendelea kuongezeka kwa kwa mahitaji ya mali salama pamoja na ununuzi dhahabu kwa benki kuu (Kielelezo 1.2). Bei ya bidhaa za kilimo ilipungua, hasa kutokana na kuongezeka kwa ugavi na kupungua kwa uhitaji katika soko la dunia. Bei ya kahawa ilishuka, ambapo bei ya Arabika ilipungua hadi dola za Marekani 8.4 kwa kilo na Robusta hadi dola za Marekani 4.2 kwa kilo, kufuatia kuongezeka kwa uga kwavi kutoka nchi zinazozalisha kahawa kwa wingi. Vilevile, bei za pamba zilipungua

kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa ugavi (Kiambatanisho, Jedwali A8).

Mfumuko wa bei katika nchi nyingi ulibakia kuwa wa chini na wenye mwelekeo wa kupungua kwa mwaka 2025. Aidha nchi nyingi zilikuwa na viwango vilivyo karibu na, au chini ya malengo ya benki kuu zao vya mfumuko wa bei (Kielelezo 1.3). Hata hivyo, katika nchi zilizoathiriwa moja kwa moja na ongezeko la ushuru wa kibiashara uliowekwa na mataifa makubwa hasa Marekani, kasi ya kupungua kwa mfumuko wa bei ilikuwa ndogo ikilinganishwa na nchi nyingine.

Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, hususani nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)—mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kukaribia viwango linganifu vya mtangamano wa kikanda, ukichangiwa na mfumuko mdogo wa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na utulivu wa jumla wa bei za vyakula na nishati katika masoko ya ndani (Kielelezo1.4 na Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects

Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**




Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu

Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Uchumi wa Ndani

Uchumi wa ndani ulikuwa imara katika robo ya tatu ya mwaka 2025, ukichangiwa na uwekezaji katika sekta ya umma na binafsi. Pato la Taifa halisi (GDP) la Tanzania bara lilikua kwa asilimia 6.4, kutoka asilimia 6.1 iliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2024, huku mchango mkubwa ukitolewa na sekta za kilimo; madini na uchimbaji wa mawe; ujenzi, pamoja na huduma za kifedha na bima (Kielelezo 2.1a na Kielelezo 2.1b).

**Kielelezo 2.1a: Ukuaji wa Uchumi kwa Robo Mwaka**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Kielelezo 2.1b: Mchango wa Baadhi ya Sekta Katika Pato la Taifa Kwa Robo Mwaka**




Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## 2.2 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.6 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwezi kama huo mwaka 2024. Hata hivyo, mfumuko huu wa bei ulibaki ndani ya wigo wa lengo la taifa la asilimia 3–5 (Jedwali 2.2.1 and Kielelezo 2.2.1). Kiwango hicho kilikuwa ndani ya vigezo vya mtangamano wa kikanda wa EAC na SADC vya chini ya asilimia 8 na wigo wa asilimia 3-7, mtawalia ( Kielelezo 2.2.2). Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa mfumuko wa bei wa chakula, pamoja na kuongezeka kwa matumizi wakati wa msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka (Kielelezo 2.2.3). Mfumuko wa bei wa chakula uliongezeka hadi kufikia asilimia 6.7, ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwezi kama huo wa mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei ya vyakula vya msingi kama vile mchele, unga wa mahindi, unga wa ngano, ulezi na mtama (Kielelezo 2.2.4a na Kielelezo 2.2.4b).

**Jedwali 2.2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

| | | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Des-24 | Nov-25 | Des-25 | Des-24 | Nov-25 | Des-25 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 1.9 | 0.4 | 2.0 | 4.6 | 6.6 | 6.7 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.5 | 0.1 | 0.4 | 2.2 | 3.5 | 3.4 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 1.2 | 2.0 | 2.0 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.3 | -0.2 | 0.5 | 2.9 | 2.2 | 2.3 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 2.1 | 3.0 | 3.0 |
| Afya | 2.5 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 1.9 | 1.3 | 1.3 |
| Usafiri | 14.1 | 0.2 | 1.3 | 1.4 | 3.5 | 2.9 | 4.1 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 1.0 | 0.3 | 0.5 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.1 | -0.2 | -0.1 | 2.0 | 0.4 | 0.3 |
| Elimu | 2.0 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 3.2 | 3.0 | 2.9 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 2.8 | 1.0 | 0.9 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.0 | -0.1 | 0.1 | 1.1 | 0.3 | 0.4 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.2 | 0.3 | -0.3 | 5.3 | 1.7 | 1.2 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | 0.7 | 0.3 | 0.9 | 3.1 | 3.4 | 3.6 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.3 | 0.5 | 0.4 | 3.3 | 2.3 | 2.5 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | 1.7 | -0.1 | 2.2 | 3.3 | 6.2 | 6.7 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | 0.5 | -0.5 | 1.3 | 5.3 | 3.8 | 4.6 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | 0.1 | 0.6 | 0.5 | 1.6 | 1.6 | 2.0 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 1.1 | 0.2 | 1.2 | 3.8 | 4.4 | 4.5 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 0.2 | 0.1 | -0.1 | 2.9 | 2.4 | 2.2 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.2 | 0.3 | 0.5 | 2.5 | 2.1 | 2.3 |

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.1: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili




Chanzo: Wizara ya viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.2: Mfumuko wa Bei na Malengo yake

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.3: Mchango Katika Mfumuko wa Bei




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.4: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao

#### a. Mazao ya Vyakula Vikuu

Asilimia




Chanzo: Wizara ya viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

#### b. Mazao ya Vyakula Mbadala

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula kinachohifadhiwa na Wakala wa Kitaifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) nchini ilikuwa tani 577,376 mwezi Desemba 2025, kufuatia ununuzi ya tani 49.9 na mauzo ya tani 13,098.2 za mahindi kwa wafanya biashara mbalimbali nchini (Jedwali 2.2.2). Uuzaji wa chakula uliendelea kusaidia utulivu wa bei za vyakula masokoni.

**Jedwali 2.2.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 110,398 | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 |
| Feb | 110,389 | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 |
| Mac | 109,231 | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 |
| Apr | 109,231 | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 |
| Mei | 108,284 | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 |
| Jun | 107,384 | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 |
| Jul | 107,384 | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 |
| Ago | 123,635 | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 |
| Sep | 150,057 | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 |
| Okt | 192,408 | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 |
| Nov | 209,057 | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 |
| Des | 214,968 | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Mfumuko wa bei za msingi (core inflation) ulipungua hadi asilimia 2.5 mwezi Desemba 2025 kutoka asilimia 3.3 mwezi kama huo mwaka 2024. Mwenendo huu unaashiria kushuka kwa bei za bidhaa zilizochakatwa kama mafuta ya alizeti, sukari, gesi ya kupikia na sare za shuleni na huduma ya usafiri wa mwendo mfupi[2].

Mfumuko wa bei katika kundi la nishati, mafuta na huduma za umma (public utilities) ulipungua hadi asilimia 4.6 mwezi Desemba 2025 kutoka asilimia 5.3 mwezi kama huo mwaka jana. Hali hii ilichangiwa zaidi na kupungua kwa kasi ya bei za petroli na mafuta ya taa, jambo lililoakisi kushuka kwa bei za mafuta katika masoko ya dunia (Kielelezo 2.2.5).

**Kielelezo 2.2.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa Lita




Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu

## 2.3 Sera ya Fedha

Kikao chake cha 239 cha mwezi Oktoba 2025, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate-CBR) kuendelea kuwa asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Desemba, 2025. Uamuzi huu ulilenga kuendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi huku matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3-5. Sambamba na uamuzi huo, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki (Interbank Cash Market-IBCM) inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/-2 ya riba ya Benki Kuu (CBR).

Katika mwezi Desemba 2025, utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha. Hali ya ukwasi katika sekta ya benki ilikua ya kutosha, huku riba ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki (IBCM) ikibaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.3.1). Mafanikio haya yalitokana na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu kwa kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki (Reverse repo) yenye thamani ya Shilingi bilioni 1,419.3 na hivyo kupelekea kiwango cha ukwasi kuwa cha kutosha kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi (Kielelezo 2.3.2).

[2] https://www.nbs.go.tz/statistics/topic/consumer-price-index-2015-2

### Kielelezo 2.3.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.3.2: Mikopo Ya Muda Mfupi Kwa Mabenki




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulifikia asilimia 25.8 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 22.9 kwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.3.3 na Jedwali 2.3.1). Ukuaji huu kwa kiwango kikubwa ulitokana na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi ambayo ilikua kwa asilimia 23.5, ikilinganishwa na asilimia 18.1 kwa mwezi uliopita (Kielelezo 2.3.4 na Kielelezo 2.3.5).

### Kielelezo 2.3.3: Mwenendo Wa Ujazi Wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Jedwali 2.3.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| | Kiasi (Shilingi Billioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipengele** | Des-24 | Nov-25 | Des-25 | Des-24 | Nov-25 | Des-25 |
| Rasilimali halisi za nje | 13,558.2 | 16,298.6 | 15,283.5 | 20.0 | 22.6 | 12.7 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 11,863.4 | 13,892.1 | 13,707.3 | -1.8 | 21.4 | 15.5 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,694.8 | 2,406.5 | 1,576.1 | --- | --- | --- |
| Rasilimali halisi za ndani | 35,346.8 | 44,560.0 | 46,240.8 | 8.1 | 23.0 | 30.8 |
| Madai rasmi ya ndani | 47,559.0 | 57,629.3 | 57,160.1 | 9.4 | 17.6 | 20.2 |
| Amana za Serikali zilizopo Ben | 8,092.0 | 9,303.8 | 9,607.6 | -6.4 | 16.4 | 18.7 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,097.4 | 43,385.5 | 44,584.6 | 12.4 | 18.1 | 23.5 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,212.2 | -13,069.3 | -10,919.3 | 13.6 | 2.3 | -10.6 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 48,905.0 | 60,858.6 | 61,524.3 | 11.1 | 22.9 | 25.8 |
| Amana za fedha za kigeni | 11,765.3 | 14,056.5 | 13,381.1 | 17.6 | 13.9 | 13.7 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 37,139.7 | 46,802.2 | 48,143.2 | 9.2 | 25.9 | 29.6 |
| Amana zinginezo | 14,234.2 | 17,618.1 | 17,944.2 | 6.2 | 22.7 | 26.1 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 22,905.5 | 29,184.1 | 30,199.0 | 11.2 | 27.9 | 31.8 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 7,351.6 | 8,545.0 | 8,492.3 | 13.4 | 12.5 | 15.5 |
| Amana za hundi | 15,553.9 | 20,639.0 | 21,706.7 | 10.2 | 35.6 | 39.6 |
| Fedha za msingi (M0) | 12,024.5 | 15,135.7 | 14,508.3 | 19.1 | 27.6 | 20.7 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.3.4: Mabadiliko Katika Vyanzo Vya Ujazi Wa Fedha Kwa Mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.3.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

**Kielelezo 2.3.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa mikopo ulikuwa mkubwa zaidi katika sekta ya madini kwa asilimia 91.1 mwezi Desemba 2025, ikifuatiwa na biashara na kilimo zilizokua kwa asilimia 49.7 na 28.9, mtawalia (Jedwali 2.3.2). Mikopo kwa shughuli binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika kugharamia shughuli za wajasiriamali wadogo sana, wadogo na wa kati iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote iliyoelekezwa kwenye sekta binafsi, asilimia 35.8, ikifuatiwa na biashara kwa asilimia 15.3 na kilimo, asilimia 13.2 (Kielelezo 2.3.6).

**Jedwali 2.3.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia

| | Des-24 | Mac-25 | Jun-25 | Sep-25 | Nov-25 | Des-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | -36.3 | -24.8 | 20.8 | 32.4 | 30.1 | 91.1 |
| Biashara | 5.6 | 12.7 | 21.3 | 24.8 | 29.4 | 49.7 |
| Kilimo | 41.0 | 36.3 | 30.2 | 27.6 | 27.0 | 28.9 |
| Ujenzi | 11.6 | 35.1 | 25.7 | 15.7 | 22.4 | 25.6 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 13.2 | 22.4 | 25.7 | 17.4 | 22.1 | 29.4 |
| Hoteli na migahawa | 2.7 | 5.4 | 22.5 | 16.3 | 19.4 | 2.5 |
| Shughuli binafsi | 14.7 | 9.4 | 13.7 | 14.7 | 10.3 | 17.7 |
| Viwanda | 16.3 | 10.9 | 2.5 | 0.1 | 2.8 | -8.2 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Viwango vya Riba

Riba za mikopo na amana zilipungua kidogo mwezi Desemba, 2025. Wastani wa riba za mikopo ulipungua kidogo hadi kufikia asilimia 15.24, kutoka asilimia 15.27 kwa mwezi uliotangulia. Vilevile, riba za mikopo ya wateja wakubwa (negotiated lending rates) zilipungua kidogo hadi asilimia 12.38 ikilinganishwa na asilimia 12.61 ya mwezi Novemba 2025. Wastani wa riba za amana, ulikuwa asilimia 8.36, chini kidogo ya asilimia 8.54 kwa mwezi uliopita huku kiwango cha riba za amana kinachotolewa kwa wateja wakubwa kikiwa asilimia 11.6 karibu sawa na mwezi Novemba 2025. Kufuatia mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.88, kutoka asilimia 6.12, mwezi kama huo mwaka 2024 (Jedwali 2.4.1).

**Jedwali 2.4.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Nov-24 | Mac-25 | Jun-25 | Sep-25 | Okt-25 | Nov-25 | Des-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.69 | 2.86 | 2.90 | 2.92 | 2.93 | 2.88 | 3.02 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.67 | 15.50 | 15.23 | 15.18 | 15.19 | 15.27 | 15.24 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.56 | 15.83 | 15.69 | 15.52 | 15.50 | 15.53 | 15.46 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.77 | 12.94 | 12.68 | 12.84 | 12.40 | 12.61 | 12.38 |
| Riba za amana -jumla | 8.18 | 8.00 | 8.74 | 8.50 | 8.36 | 8.54 | 8.36 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.63 | 8.14 | 9.79 | 9.84 | 9.21 | 10.02 | 9.58 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.14 | 10.35 | 11.21 | 11.05 | 11.22 | 11.67 | 11.66 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 5.93 | 7.69 | 5.90 | 5.69 | 6.28 | 5.51 | 5.88 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.5 Masoko ya Fedha

### Soko la dhamana za Serikali

Kwa mwezi Desemba 2025, Benki Kuu iliendesha mnada mmoja wa dhamana za Serikali wenye thamani ya shilingi bilioni 176.1, kwa lengo hasa la kugharamia matumizi ya Serikali na utekelezaji wa sera ya fedha. Sanjari na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, mnada huo ulipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 341.2 (Oversubscribed), ambapo shilingi bilioni 291.7 zilikubaliwa. Kufuatia mwenendo huu, riba za dhamana za Serikali zilipungua kidogo hadi asilimia 5.87 kutoka asilimia 6.25 mwezi uliotangulia.

**Kielelezo 2.5.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki iliendesha mnada wa hati fungani ya miaka 20, wenye thamani ya shilingi bilioni 236.3. Mnada huo ulipokea kiasi kikubwa cha zabuni kuliko ilivyotarajiwa(oversubscription), ikiashiria wawekezaji wengi kupendelea hati fungani za muda mrefu. Mnada huu ulipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 813.5, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 232.9 zilikubaliwa. Riba katika mnada huo ilipungua hadi asilimia 12.02 hali inayoashiria kuimarika kwa mazingira ya utoaji wa mikopo na kuendelea kuaminika kwa soko la mikopo la ndani.

### Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya benki (IBCM) liliendelea kutumika katika kusambaza ukwasi baina ya mabenki. Katika mwezi Desemba, 2025 soko la fedha baina ya benki liliimarika ambapo jumla ya mauzo katika soko yaliongezeka hadi shilingi bilioni 3,481.9 kutoka shilingi bilioni 1,781.0 mwezi uliotangulia na shilingi bilioni 1,616.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.5.2). Mikopo ya siku saba ilichukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikiwa na asilimia 39.9. Wastani wa riba katika soko haukuwa na mabadiliko makubwa ambapo ilifikia asilimia 6.29 ikilinganishwa na asilimia 6.30 kwa mwezi uliotangulia.

**Kielelezo 2.5.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Soko la fedha za kigeni

Hali ya soko la fedha za kigeni iliendelea kuwa tulivu mwezi Desemba 2025, ikichangiwa na mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa za huduma nje ya nchi. Kufuatia mwenendo huu, mauzo ya fedha za kigeni yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 178.6 kutoka dola za Marekani milioni 158.68 mwezi uliotangulia ambapo asilimiaa 88.3 ya mauzo haya yalifanywa na benki za biashara (Kielelezo 2.5.3). Benki Kuu ilishiriki kwa kuuza dola za Marekani milioni 87.75, kwa mujibu wa sera ya ushiriki katika soko la fedha za kigeni.

Sambamba na kuongezeka kwa hali ya ukwasi wa fedha za kigeni, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,452 kwa dola moja ya Marekani kwa mwezi Desemba, ikilinganishwa na Shilingi 2,444.81 kwa dola moja ya Marekani mwezi uliotangulia. Kwa mwaka unaoishia Desemba, 2025 thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 1.3 ikilinganishwa na ongezeko la thamani kwa asilimia 3.8 iliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2024.

**Kielelezo 2.5.3: Mwenendo wa Soko la fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.6 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Makusanyo ya mapato ya ndani mwezi Novemba 2025 yalifikia shilingi bilioni 3,087.9, sawa na asilimia 2.3 chini ya lengo la mwezi husika. Serikali kuu ilikusanya shilingi bilioni 2,981.8, ikiwa chini ya lengo kwa asilimia 1.2, huku mapato yaliyosalia yakitokana na mamlaka za serikali za mitaa kupitia vyanzo vyao vya ndani.

Mapato ya kodi mwezi Novemba 2025 yalifikia shilingi bilioni 2,614.5, sawa na ongezeko la asilimia 1.7 juu ya lengo la mwezi, ikiashiria athari chanya za maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 367.3, ambayo ni chini ya lengo la shilingi bilioni 448.9 (Kielelezo 2.6.1).

**Kielelezo 2.6.1: Mapato ya Serikali kuu Mwezi Novemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato. Jumla ya matumizi ya Serikali katika mwezi Novemba 2025 yalifikia shilingi bilioni 3,780.5, ambapo shilingi bilioni 2,449.1 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 1,331.4 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.6.2).

**Kielelezo 2.6.2: Matumizi ya Serikali kuu Mwezi Novemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

## 2.7 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 50,794.2 mwishoni wa mwezi Desemba 2025, likipungua kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa Novemba 2025. Kati ya kiasi hicho, asilimia 69.5 ilikuwa ni deni la nje.

### Deni la nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 0.5 mwezi Desemba 2025 kutoka mwezi Novemba 2025, na kufikia dola za Marekani milioni 35,309.2. Katika kiasi hicho, asilimia 82.8 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.7.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Disemba 2025 ilikuwa dola za Marekani milioni 191.1, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 183.5 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni

136.8 zilitumika kufanya malipo ya deni la msingi.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji haukua na mabadiliko makubwa, huku mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu kwa asilimia 58.2 ya deni lote, wakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.7.2). Aidha, mgawanyo wa kisekta wa mikopo unaonesha kuwa mikopo ya urari wa malipo ya nje na utekelezaji wa bajeti (BOP and budget support) iliongoza kwa kwa asilimia 22.4 ikifuatiwa na mikopo kwenda kwenye shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66.0, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya, Euro (Jedwali 2.7.3 na 2.7.4).

### Jedwali 2.7.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji

Dola za Marekani Milioni

| | Dis-24 | | Nov-25[r] | | Dis-25[p] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Serikali Kuu | 25,877.1 | 80.9 | 29,109.3 | 82.9 | 29,232.6 | 82.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 25,799.9 | 80.6 | 29,030.3 | 82.6 | 29,152.5 | 82.6 |
| Malimbikizo ya riba | 77.2 | 0.2 | 79.0 | 0.2 | 80.1 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,116.3 | 19.1 | 6,012.6 | 17.1 | 6,072.9 | 17.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,566.1 | 17.4 | 5,645.8 | 16.1 | 5,650.7 | 16.0 |
| Malimbikizo ya riba | 550.2 | 1.7 | 366.8 | 1.0 | 422.2 | 1.2 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 31,997.1 | 100.0 | 35,125.7 | 100.0 | 35,309.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

### Jedwali 2.7.2: Mchanganuo wa deni la nje kwa kundi la wakopeshaji

Dola za Marekani Milioni

| | Dis-24 | | Nov-25[r] | | Dis-25[p] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,145.8 | 56.7 | 20,331.8 | 57.9 | 20,544.3 | 58.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,114.9 | 56.6 | 20,298.1 | 57.8 | 20,507.4 | 58.1 |
| Malimbikizo ya riba | 30.9 | 0.1 | 33.8 | 0.1 | 37.0 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,270.3 | 4.0 | 1,508.0 | 4.3 | 1,513.5 | 4.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,193.2 | 3.7 | 1,428.9 | 4.1 | 1,433.4 | 4.1 |
| Malimbikizo ya riba | 77.2 | 0.2 | 79.0 | 0.2 | 80.1 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,459.7 | 35.8 | 12,579.8 | 35.8 | 12,538.0 | 35.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,111.6 | 34.7 | 12,289.5 | 35.0 | 12,201.8 | 34.6 |
| Malimbikizo ya riba | 348.1 | 1.1 | 290.3 | 0.8 | 336.2 | 1.0 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,121.3 | 3.5 | 706.1 | 2.0 | 713.4 | 2.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 950.1 | 3.0 | 663.4 | 1.9 | 664.4 | 1.9 |
| Malimbikizo ya riba | 171.2 | 0.5 | 42.7 | 0.1 | 49.0 | 0.1 |
| Jumla ya deni la nje | 31,997.1 | 100.0 | 35,125.7 | 100.0 | 35,309.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

### Jedwali 2.7.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia

| Shughuli ya uchumi | Dis-24 | Nov-25[r] | Dis-25[p] |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 20.4 | 22.9 | 22.8 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.3 | 21.8 | 21.7 |
| Kilimo | 4.9 | 5.2 | 5.3 |
| Nishati na madini | 12.9 | 11.9 | 12.0 |
| Viwanda | 3.5 | 3.7 | 3.6 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.0 | 19.4 | 19.4 |
| Fedha na bima | 4.6 | 3.7 | 3.7 |
| Utalii | 1.6 | 1.7 | 1.7 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Mengineyo | 5.7 | 4.7 | 4.7 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali.

### Jedwali 2.7.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia

| Sarafu | Dis-24 | Nov-25[r] | Dis-25[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.1 | 66.2 | 66.0 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.6 | 17.6 | 17.7 |
| Yuan ya China | 6.4 | 6.4 | 6.5 |
| Sarafu nyinginezo | 9.9 | 9.8 | 9.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la ndani

Deni la ndani la Serikali lilipungua kwa asilimia 1.2 na kufikia shilingi bilioni 37,898.98 mwisho wa mwezi Desemba 2025 (Kielelezo 2.7.1). Sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali ilibakia kuwa hati fungani, huku benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii vikiendelea kuwa wadai wakuu karibia asilimia 56 ya deni lote (Jedwali 2.7.5 na 2.7.6).

### Kielelezo 2.7.1: Deni la ndani la Serikali kuu

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

### Jedwali 2.7.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa vyanzo vya mikopo

Shilingi Bilioni

| | Dis-24 | | Nov-25 | | Dis-25[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 28,664.3 | 87.8 | 32,976.5 | 86.0 | 33,012.5 | 87.1 |
| Dhamana za serikali za muda mf | 2,108.0 | 6.5 | 2,082.5 | 5.4 | 1,951.9 | 5.2 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mr | 26,369.1 | 80.8 | 30,758.2 | 80.2 | 30,924.8 | 81.6 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 3,985.0 | 12.2 | 5,384.8 | 14.0 | 4,886.5 | 12.9 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 3,966.6 | 12.1 | 5,384.8 | 14.0 | 4,886.5 | 12.9 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 32,649.3 | 100.0 | 38,361.3 | 100.0 | 37,899.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

### Jedwali 2.7.6: Deni la ndani la Serikali kuu kwa kundi la wakopeshaji

Shilingi Bilioni

| | Dis-24 | | Nov-25 | | Dis-25[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,784.9 | 30.0 | 11,046.1 | 28.8 | 10,979.6 | 29.0 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 5,926.7 | 18.2 | 7,193.5 | 18.8 | 6,695.2 | 17.7 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 8,988.7 | 27.5 | 10,276.8 | 26.8 | 10,352.2 | 27.3 |
| Kampuni za bima | 1,897.2 | 5.8 | 2,008.8 | 5.2 | 2,006.1 | 5.3 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 458.2 | 1.4 | 749.8 | 2.0 | 737.8 | 1.9 |
| Wengine | 5,593.7 | 17.1 | 7,086.3 | 18.5 | 7,128.0 | 18.8 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 32,649.3 | 100.0 | 38,361.3 | 100.0 | 37,899.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Desemba 2025, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 247.8, kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana za Serikali, kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti, ambapo Shilingi bilioni 166.6 ni hati fungani na shilingi bilioni 81.2 ni dhamana za Serikali za muda mfupi (Kielelezo 2.7.2). Aidha, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 488.01 kulipia deni la ndani, ambapo shilingi bilioni 211.8 zilitumika kulipa deni la msingi na shilingi bilioni 276.2 ni malipo ya riba.

### Kielelezo 2.7.2: Dhamana za Serikali zilizotolewa kwa madhumuni ya ufadhili wa bajeti

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.8 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuimarika mwaka 2025, hali iliyoakisi kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida hadi dola za Marekani milioni 2,015.5 kutoka dola za Marekani milioni 2,379.8 zilizorekodiwa mwaka 2024 (Jedwali 2.8.1). Kuimarika huku kulichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya nje ya bidhaa na huduma ikilinganishwa na uagizaji, ambapo kwa kiasi kikubwa kimechangiwa na uagizaji wa bidhaa za kati na bidhaa mtaji zinazohusiana na shughuli za uzalishaji na uwekezaji.

Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 6,329 mwishoni mwa Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,546.9 mwishoni mwa Desemba 2024. Kiwango hiki kilitosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.9 ya makadirio ya uagizaji, ambayo ni juu ya lengo la kitaifa na mtangamano wa EAC (Kielelezo 2.8.1).

**Jedwali 2.8.1 Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali**

Dola za Marekani Milioni

| | Dec-24 | Nov-25 | Dec-25 | Mwaka ulioishia Desemba 2023 | 2024 | 2025p | Mabadiliko ya asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa bidhaa | -388.8 | -158.9 | -319.3 | -6,032.3 | -5,074.0 | -4,399.4 | -13.3 |
| Zilozouzwa nje* | 951.5 | 1,098.5 | 1,059.8 | 7,696.6 | 9,121.6 | 10,282.4 | 12.7 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,340.2 | 1,257.4 | 1,379.1 | 13,728.9 | 14,195.6 | 14,681.8 | 3.4 |
| Urari wa huduma | 435.69 | 320.5 | 337.3 | 3,835.9 | 4,051.7 | 4,172.5 | 3.0 |
| Mapato | 696.7 | 593.9 | 626.1 | 6,231.7 | 6,846.8 | 7,316.8 | 6.9 |
| Malipo | 261.0 | 273.4 | 288.8 | 2,395.9 | 2,795.0 | 3,144.4 | 12.5 |
| Urari wa bidhaa na huduma | 46.9 | 161.6 | 18.0 | -2,196.5 | -1,022.3 | -227.0 | -77.8 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,648.1 | 1,692.4 | 1,685.8 | 13,928.3 | 15,968.4 | 17,599.2 | 10.2 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,601.2 | 1,530.8 | 1,667.8 | 16,124.8 | 16,990.7 | 17,826.1 | 4.9 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -181.8 | -166.4 | -199.0 | -1,496.6 | -1,887.4 | -2,072.1 | 9.8 |
| Yaliyoingia | 41.7 | 29.5 | 40.1 | 301.2 | 311.7 | 411.8 | 32.1 |
| Yaliyotoka | 223.5 | 195.9 | 239.1 | 1,797.7 | 2,199.2 | 2,483.9 | 12.9 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 109.3 | -5.7 | 16.6 | 732.5 | 529.9 | 283.5 | -46.5 |
| Iliyoingia | 149.0 | 57.7 | 84.2 | 1,280.9 | 1,177.4 | 851.9 | -27.6 |
| ambapo Serikali | 66.8 | 0.0 | 13.9 | 131.0 | 139.2 | 32.1 | -76.9 |
| Iliyotoka | 39.6 | 63.4 | 67.6 | 548.4 | 647.5 | 568.3 | -12.2 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -25.5 | -10.6 | -164.3 | -2,960.6 | -2,379.8 | -2,015.5 | -15.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.8.1 Akiba ya fedha za kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

## Mauzo ya nje

Mwaka 2025, mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia dola za Marekani milioni 17,599.2 kutoka dola za Marekani milioni 15,968.4 mwaka 2024. Mauzo ya nje ya bidhaa yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 10,282.4 mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 9,121.6 zilizorekodiwa mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku, na kahawa (Kielelezo 2.8.2). Mauzo ya dhahabu, ambayo yalichangia asilimia 45.7 ya jumla ya mauzo ya nje ya bidhaa, yaliongezeka kwa asilimia 37.4 na kufikia dola za Marekani milioni 4,697.6, kutokana na bei nzuri katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji. Mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,548.6 kutoka dola za Marekani milioni 1,341.3 mwaka 2024.

Mauzo ya bidhaa asilia yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,512.2 mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 1,473.3 mwaka 2024. Ukuaji huu ulitokana zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya tumbaku na kahawa, yaliyochochewa na kuongezeka kwa bei na kiwango cha mauzo. Mauzo ya nje ya bidhaa kwa mwezi yalifikia dola za Marekani milioni 1,059.8 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 951.5 mwezi Desemba 2024, kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya nje ya dhahabu na bidhaa za viwandani.

**Kielelezo 2.8.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa kiasi kikubwa hadi kufikia dola za Marekani milioni 7,316.8 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 6,846.8 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na kuongezeka kwa mapato ya huduma za utalii na usafirishaji. Mapato ya huduma za utalii yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,948.2 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024, ikiwa ni sambamba na ongezeko la asilimia 7.1

la idadi ya watalii waliofikia 2,294,495. Mapato ya huduma za usafirishaji yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,796.5 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 2,353.4 mwaka 2024, yakichangiwa zaidi na ongezeko la mapato ya usafirishaji wa bidhaa (Kielelezo 2.8.3). Kwa mwezi, mapato ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 626.1 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 696.7 mwezi Desemba 2024. Mwelekeo huu unatofautiana na mwenendo wa mwaka.

**Kielelezo 2.8.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

## Uagizaji wa bidhaa na huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka hadi dola za Marekani milioni 17,826.1 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9 kutoka dola za Marekani milioni 16,990.7 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na uagizaji wa bidhaa za viwandani, huduma za usafirishaji, vifaa vya usafiri viwandani, pamoja na mashine na mitambo, ambavyo kwa kiasi kikubwa ni bidhaa mtaji na kati. Uagizaji wa mafuta ulipungua kwa asilimia 6.7 hadi dola za Marekani milioni 2,380.1 kutoka dola za Marekani milioni 2,552.3. Hali inaashiria kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia (Kielelezo 2.8.4). Kwa ulinganifu wa kila mwezi, uagizaji wa bidhaa ulifikia dola za Marekani milioni 1,379.1 mwezi Desemba 2025, kutoka dola za Marekani milioni 1,340.2 mwezi Desemba 2024.

**Kielelezo 2.8.4: Ulinganifu wa Uagizaji wa bidhaa na huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi p inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 12.5 hadi dola za Marekani milioni 3,144.4 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 2,795 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa malipo ya usafirishaji, ambayo ni sambamba na mwenendo wa uagizaji bidhaa za nje (Kielelezo 2.8.5). Kwa ulinganifu wa kila mwezi, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 288.8 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 261 mwezi Desemba 2024.

**Kielelezo 2.8.5: Malipo ya huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo:Ukokotoaji wa Benki kuu ya Tanzania
Tanbihi:Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano ya simu, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za kiserikali,huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi kwa mwaka 2025 iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,072.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,887.4 mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa malipo ya mapato yatokanayo na umiliki wa mtaji (hisa) na riba. Kwa ulinganifu wa kila mwezi, nakisi ya mapato ya vitega uchumi yalifikia dola za Marekani milioni 199 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 181.8 mwezi Desemba 2024.

